TANGAZO LA SERIKALI Na. 826 la tarehe. 4/10/2024

SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI,
(SURA YA 20)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 205)*

AMRI YA UTEUZI WA MTAALAM WA MAANDISHI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uteuzi wa Mtaalam wa Maandishi ya mwaka 2024.

Uteuzi wa mtaalam wa Maandishi

**2**. Mtu ambaye jina lake limetajwa katika Jedwali anateuliwa kuwa Mtaalam wa Maandishi kwa madhumuni ya kutoa ripoti kama ushahidi katika mashauri yoyote ya jinai au masuala yanayohusiana na hayo.

Uhalali wa uteuzi

**3**.-(1) Uteuzi uliofanywa chini ya Aya ya 2 utakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Amri hii.

(2) Bila ya kujali masharti ya aya ndogo ya (1), mtu aliyeteuliwa kama mtaalam wa Maandishi anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi kisichofikia miaka mitano endapo-

(a) ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma imekoma; au

(b) uteuzi wake kama Mtaalam wa maandishi umesitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | JINA |
|---|---|
| 1. | Edson Jackson |
| 2. | Abdulkarim Hussein |

Dodoma,
24 Septemba, 2024

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU,
*Mkurugenzi wa Mashtaka*